**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

# MKUTANO WA TATU

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA THELATHINI NA NNE

**1 JUNI, 2016**

**MKUTANO WA TATU - YATOKANAYO NA KIKAO CHA THELATHINI NA NNE**

**TAREHE 1 JUNI, 2016**

## I. DUA:

Saa 3.00 Asubuhi Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) alisoma Dua na Kuongoza Bunge.

**Makatibu Mezani:**

1. Ndg. Charles Mloka
2. Ndg. Lawrence Makigi

Baada ya kusoma Dua Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani walitoka nje na kumwacha Mhe. David Ernest Silinde

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani:

1. Naibu Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Mezani Hotuba ya Bajeti ya Wizara yake kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

2. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti aliwasilisha Mezani Taarifa ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

3. Mhe. David Ernest Silinde aliwasilisha Mezani Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

   Mhe. David Silinde alitoka nje ya Ukumbi mara baada ya kuwasilisha Mezani Taarifa ya Upinzani .

## III. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Swali Na.275 – Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab
Swali la nyongeza: Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Swali Na.276 – Mhe. Amina Saleh Mollel [kny. Sabreena Hamza Sungura]
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Amina Saleh Mollel
(ii) Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwanko

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Swali Na.277 – Mhe. Abdallah Dadi Chikota [kny. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia]
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Abdallah Dadi Chikota
(ii) Mhe. Zaynabu Matitu Vullu

Swali Na.278 – Mhe. Jerome Dismass Bwanausi
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Jerome Dismass Bwanausi
(ii) Mhe. Joseph Kasheku Musukuma
(iii) Mhe. Oliver Daniel Semguruka
(iv) Mhe. Zacharia Paulo Issaay

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

Swali Na.279 – Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Dalaly Peter Kafumu
(ii) Mhe. Margareth Simwanza Sitta
(iii) Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda
(iv) Mhe. Martha Moses Mlata

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Swali Na.280 – Mhe. Subira Khamis Mgalu [kny. Mhe. Munira Mustafa Khatib]
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Subira Khamis Mgalu
(ii) Mhe. Constantine John Kanyasu

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

Swali Na.281 – Mhe. Mattar Ali Salum
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Mattar Ali Salum
(ii) Mhe. Shabani Omar Shekilindi

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**
Swali Na.282 – Mhe. Sixtus Raphael Mapunda [kny. Mhe. John John Mnyika]
Swali la nyongeza: Mhe. Sixtus Raphael Mapunda

Swali Na.283 – Mhe. Ally Saleh Ally
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Ally Saleh Ally
(ii) Mhe. Edward Franz Mwalongo

**MATANGAZO:**

- Wageni wote walioko Bungeni walitambulishwa;

- Mkutano wa Bunge Sports Club utafanyika saa 7.00 mchana katika maeneo ya Bunge kwa ajili ya uchaguzi wa viongozi.

- Ibada ya Misa Takatifu iliyoandaliwa na Jumuiya ya Mt. Thomas Moore kwa wakatoliki na waumini wengine wa kikristo itakafanyika saa 7 mchana katika maeneo ya Bunge.

## IV. TAARIFA YA NAIBU SPIKA:

Naibu Spika alitoa Taarifa kuhusu mauaji ya kutisha yaliyotokea hivi karibuni Mkoani Tanga na kulieleza Bunge kuwa, kutokana na mauaji hayo Serikali imemtuma Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwenda Mkoani Tanga kufanya uchunguzi wa kina na kupata taarifa ya kiini cha mauaji hayo.

Aidha, aliagiza kuwa Serikali ishughulikie suala hili mapema iwezekanavyo na kuwasilisha Taarifa Bungeni ili kuwajulisha Wabunge kuhusu mauaji hayo.

## V. MWONGOZO WA SPIKA:

Mhe. Martha Moses Mlata aliomba Mwongozo chini ya Kanuni ya 68(7) akiomba maelekezo ya Kiti kuhusu hali inayojitokeza Bungeni wakati baadhi ya Mawaziri wanapojibu maswali ya Wabunge kutumia muda mwingi na kupoteza muda bila kutoa majibu yenye kueleweka. Alitaka kujua ni utaratibu gani utumike ili kuwawezesha wawe na majibu mafupi yanayoeleweka na yaliyo sahihi.

Naibu Spika aliahidi kutoa majibu ya mwongozo huo baadae.

Mhe. Kangi Alphaxard Lugora aliomba Mwongozo chini ya Kanuni ya 68(7) na kueleza kusikitishwa kwake kuhusu mauaji yanayoendelea nchini hivi sasa akitolea mfano wa mauaji yaliyotokea Mwanza na Tanga kuwa yana viashiria vya mauaji ya kigaidi au yaliyopangwa (*organized crime*). Aidha, alisema kuwa licha ya Bunge kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu namna ya kukabiliana na matatizo

hayo, bado yamekuwa yakijirudia. Alitaka kujua Serikali ina mkakati gani kuhusu mauaji hayo.

Naibu Spika alimwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mhe. Jenista Mhagama ili kutoa taarifa.

Waziri wa Nchi, alilieleza Bunge kuwa Serikali inafahamu kuwepo kwa matatizo haya; na kwamba Waziri Mkuu amekwishatoa maelekezo ndani ya Serikali jinsi ya kuyashughulikia. Pamoja na hayo, licha ya Naibu Waziri kutumwa kwenda kwenye maeneo ya tukio, alisema kuwa jambo hili si jepesi kiasi cha kutoa jibu bila kufuatilia kwanza undani wake na kwamba si sahihi kuyachukulia moja kwa moja kuwa ni mauaji ya kigaidi.

Waziri wa Nchi aliliomba Bunge liiachie Serikali ifanye kazi yake na pindi itakapopata taarifa za kina na sahihi itawasilisha taarifa Bungeni.

Baada ya maelezo ya Waziri, Naibu Spika alisisitiza na kuelekeza kuwa Serikali iendelee kulifanyia kazi na kuliletea Bunge taarifa kamili, wakati huo huo akiwaomba Waheshimiwa Wabunge wavute subira wakati Serikali ikilishughulikia suala hilo.

## VI. MISWADA YA SHERIA:

Miswada ya Sheria ifuatayo ilisomwa Bungeni mara ya kwanza:-

1) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2016 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2016.*

2) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2016 (*The Written Laws – Miscellaneous).*

   Baada ya Miswada hiyo kusomwa Mara ya Kwanza, Naibu Spika alitamka rasmi kuwa Miswada hiyo imesomwa mara ya kwanza na kwamba hatua inayofuatia ni Miswada hiyo kupelekwa kwenye Kamati zinazohusika kushughulikiwa. Aidha, alielekeza Waheshimiwa Wabunge wapitie kwenye masanduku yao ya nyaraka (*pigeon holes*) kuchukua nakala za miswada hiyo.

## VII. HOJA ZA SERIKALI:

- Naibu Spika alimwita Waziri wa Fedha na Mipango kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kuliomba Bunge kujadili na kupitisha Makadirio hayo.

- Baada ya Waziri wa Fedha na Mipango kuwasilisha Makadirio yake, Naibu Spika alimwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kuwasilisha Taarifa ya Kamati kwa Mujibu wa Kanuni ya 99(9).

- Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango, Mhe. David Ernest Silinde, aliwasilisha Taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9). Hata hivyo, hakuwa tayari kuisoma taarifa hiyo kwa kile alichodai kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani hairidhishwi na mwenendo wa Naibu Spika dhidi yao. Pamoja na hayo aliomba hotuba nzima iingizwe kwenye kumbukumbu za majadiliano ya Bunge (Hansard) kama ilivyo.

- Mjadala wa jumla ulifuata na Naibu Spika aliwaita Wabunge wafuatao kuchangia Hoja ya Waziri wa Fedha:-

| | | |
|---|---|---|
| 1) Mhe. Peter Joseph Serukamba | - | CCM |
| 2) Mhe. Elias John Kwandikwa | - | CCM |
| 3) Mhe. Oran Manase Njeza | - | CCM |
| 4) Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma | - | CCM |
| 5) Mhe. Dkt Dalaly Peter Kafumu | - | CCM |
| 6) Mhe. Subira Khamis Mgalu | - | CCM |
| 7) Mhe. Martha Jachi Umbulla | - | CCM |

## VIII. UFAFANUZI WA NAIBU SPIKA KUHUSU MAMLAKA YA KITI NA HAKI YA MBUNGE KUKATA RUFAA KUPINGA MAAMUZI YA SPIKA:

Naibu Spika alitoa ufafanuzi kuhusu Kanuni ya 5 juu ya mamlaka ya Spika kuendesha vikao vya Bunge kwa kuzingatia Kanuni, Katiba, Sheria, Maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge, mila, desturi za Mabunge mengine, nk.

Aidha, alinukuu fasili za (2) na (3) za Kanuni hiyo zinazompa mamlaka Spika kutilia nguvu Kanuni zote za Bunge na kumtaka Mbunge yeyote anayekiuka Kanuni kujirekebisha.

Vile vile alinukuu Kanuni ya 72 inayoelezea Mamlaka ya Spika ya kusimamia utaratibu na kwamba uamuzi wake kuhusu utaratibu utakuwa wa mwisho.

Pamoja na hayo aliwakumbusha Wabunge kuhusu haki ya Mbunge kukata rufaa kupinga uamuzi wa Spika kwa kuzingatia utaratibu ulioelezwa katika fasili ya (4) (5) na (6). Kanuni ya 5. Mwisho, aliwataka Wabunge wote ambao hawaridhiki na maamuzi ya Kiti kutumia fursa hiyo.

**IX. KUSITISHA BUNGE**

Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni.

**X. BUNGE KUREJEA**

- Saa 10.00 Bunge lilirejea na kuongozwa na Naibu Spika, Mhe. Dkt. Tulia Ackson aliwapa nafasi Wabunge wafuatao ya kuchangia Hoja:-

8. Mhe. Asha Abdullah Juma - CCM
9. Mhe. Omary Tebwete Mgumba - CCM
10. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki - CCM
11. Mhe. Janet Zebedayo Mbene - CCM
12. Mhe. Almas Athumani Maige - CCM
13. Mhe. George Malima Lubeleje - CCM
14. Mhe. Ritta Enespher Kabati - CCM
15. Mhe. Khadija Hassan Abdood - CCM
16. Mhe. Andrew John Chenge - CCM
17. Mhe. Prosper Joseph Mbena - CCM
18. Mhe. Jitu Vrajlal Soni - CCM
19. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu - CCM
20. Mhe. Eng. Edwin Amandus Ngonyani - Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano
21. Mhe. George Mcheche Masaju - Mwanasheria Mkuu wa Serikali
22. Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji - Naibu Waziri wa Fedha na Mipango
23. Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango - Waziri wa Fedha na Mipango

**XI. KAMATI YA MATUMIZI:**

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Matumizi ili kupitisha Vifungu vya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Baada ya kumaliza, Bunge lilirejea, Waziri Mtoa Hoja alitoa Taarifa ya Kazi ya Kamati, Wabunge walihojiwa na kupitisha Bajeti husika.

**XII. MWONGOZO WA SPIKA:**

Mhe. Ally Mohammed Kessy aliomba Mwongozo chini ya kanuni ya 68(7) akirejea Kanuni ya 75 na 76 alielekeza kuwa Wabunge ambao wanasaini wakiingia Bungeni wakati wa vikao vya Bunge kuwa sawa na watumishi hewa. Aliomba kiti kielekeze ni hatua gani wanaweza kuchukuliwa Wabunge hao.

Naibu Spika alijibu kuwa suala hilo atalitolea mwongozo baadaye.

**MATANGAZO:**
Naibu Spika alitoa matangazo yafuatayo kabla ya kuahirisha Bunge:

i) Kikao cha Mashauriano ya Bajeti na Kamati ya Uongozi kitafanyika 2 Juni, 2016 katika Ukumbi wa Spika saa 7.00 mchana.

ii) Semina ya Wabunge wote baada ya kipindi cha maswali iliyoandaliwa na *Association of Fraud*.

iii) Bunge Sports Club kupata uongozi mpya chini ya Uenyekiti wa Mhe. William Mganga Ngeleja na Makamu Mwenyekiti Mhe. Ester Nicholas Matiko na viongozi wengine.

**XIII. KUAHIRISHA BUNGE:**
Saa 2.33 Usiku Bunge liliahirishwa hadi tarehe 2/6/2016 saa 3.00 asubuhi.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **DKT. T. D. KASHILILAH** |
| **1 JUNI, 2016** | **KATIBU WA BUNGE** |